**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BUNGE LA TANZANIA**

# TAARIFA YA KAMATI YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI, FUNGU 44 KWA MWAKA 2016/2017 NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI FUNGU 44 NA FUNGU 60 YA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

Ofisi ya Bunge,
Idara ya Kamati za Bunge,
**DODOMA**

**17 Mei, 2017**

**TAARIFA YA KAMATI YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI, FUNGU 44 KWA MWAKA 2016/2017 NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI FUNGU 44 NA FUNGU 60 YA MWAKA WA FEDHA 2017/2018**

## 1.0 UTANGULIZI:

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Bunge , Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, **Fungu 44-Viwanda** na kwa Mwaka wa fedha **2016/2017** na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara **Fungu 44-Viwanda** na **Fungu 60-Biashara na Uwekezaji** kwa Mwaka wa Fedha **2017/2018**.

**Mheshimiwa Spika**, Tanzania ya Viwanda inawezekana, Kamati inaipongeza Serikali kwa nia yake njema ya kutaka kuifanya Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kati ifikapo 2025 kwa kupitia viwanda. Kamati inaamini kuwa katika kutekeleza nia hii njema Serikali ihamasishe zaidi kuanzisha Viwanda ambavyo vinatumia zaidi malighafi zinazopatikana hapa nchini hususani malighafi zinazotokana na mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi ili kuwanufaisha Watanzania wengi kwa wakati mmoja.

Uwepo wa viwanda vya namna hiyo vitahamasisha kilimo na ufugaji kwa vile soko litakuwepo, hivyo ajira itapatikana kwenye kilimo, ufugaji na viwandani pia.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati katika kutekeleza majukumu yake**,** ilipokea na kujadili taarifa mbalimbali za Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji pamoja na Taasisi zilizo chini ya Wizara hii. Aidha, kwa mujibu wa Kanuni ya 98(1), Kamati ilipata fursa ya kutembelea Miradi ya Maendeleo inayotekelezezwa chini ya Wizara kwa lengo la kujionea hali halisi ya utekelezaji wa miradi hiyo. Kamati ilitembelea shughuli nyingine zinazohusiana na sekta ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji wakiwa wadau wa Wizara na hatimaye Wajumbe kuishauri Serikali ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (2), Kamati ilikutana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ili kupokea Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2016/2017, kuchambua na kujadili mapendekezo ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii inalenga kuliomba Bunge lako tukufu kuidhinisha maombi ya Fedha kwa ajili ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, lakini pia kutoa mapendekezo kwa Bunge lako tukufu kuhusu masuala kadhaa ambayo Kamati inaamini ni muhimu yakafanyiwa kazi.

## 2.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2016/2017 NA MATOKEO YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017.

### 2.1 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2016/2017

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuhusu utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa Fedha 2016/2017.

#### 2.1.1 Makusanyo ya Maduhuli

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilijulishwa kuwa katika mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ilipanga kukusanya jumla ya Shilingi **20,000,000,000** kutokana na ada za leseni, nyaraka za zabuni na faini ya kukiuka sheria ya leseni. Uchambuzi wa Kamati umebaini mambo yafuatayo:-

i) Katika mwaka wa fedha 2016/2017, hadi kufikia robo ya tatu ni Shilingi **10,781,488,987.18** tu sawa na asilimia **53.9** ndizo zilikuwa zimekusanywa. Kwa matokeo haya ni vigumu kufikiwa lengo la makusanyo ya shilingi **20,000,000,000** ifikapo tarehe 30 Juni, 2017.

ii) Lengo lilikuwa ni kukusanya asilimia **24.4** ya bajeti iliyopitishwa katika Mwaka wa Fedha **2016/2017** tofauti na mwaka uliotangulia ambapo lengo lilikuwa ni kukusanya asilimia **14.2** ya Bajeti iliyoidhinishwa.

iii) Katika Mwaka wa fedha 205/16 hadi kufikia mwezi Machi, 2016 lengo lilifikiwa kwa asilimia **74**. Ukilinganisha na mwaka wa fedha 2016/17 katika kipindi cha robo ya tatu lengo lilofikiwa ni asilimia **53** tu. Ni maoni ya kamati kuwa lengo lililowekwa halikuzingatia uwezo.

### 2.1.2 Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina.

**Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ilitengewa jumla ya shilingi **81,871,992,000.** Katika fedha hizo shilingi **41,871,992,000** zilitengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi **40,000,000,000** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, kamati ilijulishwa kuwa hadi kufikia Februari, 2017, robo ya tatu ya mwaka wa fedha Wizara ilikuwa imepokea jumla ya Shillingi **34,694,182,650** kwa ajili ya Matumizi ya Wizara na taasisi zilizopo chini yake. Kiasi hiki ni sawa na asilimia **42.4** tu ya fedha zote zilizotengwa katika Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Kati ya

fedha hizi Shilingi **27,118,672,025** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na asilimia **64.8** ya Shilingi **41,871,992,000** fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Aidha, kati ya Shilingi **27,118,672,025,** fedha zilizopelekwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida Shilingi **23,536,396,450** ni kwa ajili ya mishahara na Shilingi **3,582,275,575** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC).

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Machi, 2017, kati ya Shilingi **40,000,000,000** zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni Shilingi **7,566,620,625** tu ndizo zilikuwa zimepokelewa na Wizara, kiasi hiki ni sawa na asilimia **18.92** ya fedha zote za Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya uchambuzi wa kina wa Taarifa ya Utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa mwaka fedha **2016/2017**, Kamati ilibaini kwamba:-

i) Haikuridhishwa na mwenendo nzuri wa wa upatikanaji wa fedha kutoka Hazina jambo linalopelekea kukwama kwa utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

ii) Fedha kutoka hazina zimekuwa zikipelekwa kwa kuchelewa sana. Mfano hadi kufikia Machi, 2017 kati ya shilingi **40,000,000,000** fedha za miradi ya Maendeleo ni shilingi **7,566,620,625** tu ndizo zilikuwa zimepelekwa

na Wizara jambo hili linapelekea kuchelewa kwa utelelezaji wa miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaona kwamba ni wakati muafaka sasa kwa Serikali kubadilika na kutoa fedha kwa wakati ili kutimiza matarajio ya watanzania ya kuwa na Tanzania ya Viwanda ifikiapo 2025.

## 2.2 MATOKEO YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge toleo la Februari, 2016, katika kutekeleza majukumu yake Kamati ilifanya ziara ya kutembelea baadhi ya miradi iliyotengewa fedha na inatekelezwa na Wizara hii.

Kamati ilifanya ziara ya kutembelea baadhi ya miradi ya maendeleo kwa lengo kujionea hali halisi na hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wake. Aidha, Kamati ilitembelea shughuli za Viwanda kwa lengo la kujionea mafanikio na changamoto katika uendeshaji wa Sekta ya viwanda.

**Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha wa 2016/2017, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Fungu **44** iliidhinishiwa shilingi **9,000,000,000** kwa ajili ya kutekeleza

mradi namba **6260** unaojulikana kama *NDC-Industrial Park (TAMCO-Kibaha)* .Mradi huu ni kwa ajili ya ujenzi wa maeneo ya Viwanda.

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unatekelezwa chini ya Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC). Jukumu la Shirika la Maendeleo la Taifa katika kuanzisha miradi ya aina hii ni kutafuta ardhi ya Mradi, kujenga miundombinu inayohitajika na kuvutia wawekezaji kwa ajili ya kujenga Viwanda katika maeneo hayo. Lengo la Shirika ni kuendeleza eneo hilo kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vipya.

Mpango wa matumuzi ya ardhi katika eneo la TAMCO lenye ukubwa wa ekari **230** ni kama ifuatavyo:-

| Na | Matumizi ya Ardhi | Ukubwa (Ekari) |
|---|---|---|
| 1 | Viwanda vya nguo na mavazi (Textile and Garments) | 95 |
| 2 | Viwanda vya kuunganisha magari na mitambo mbalimbali | 64 |
| 3 | Viwanda vya Kibaiolojia na Vifaa-tiba | 43 |
| 4 | Huduma mbalimbali za uzalishaji | 5 |
| 5 | Mabwawa ya kutibu maji taka (oxidation ponds) | 5 |
| 6 | Barabara na maegesho ya magari | 18 |

**Mheshimiwa Spika**, hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa mradi ni kukamilika kwa mpango wa matumizi ya ardhi (Land

Use Plan) na upimaji wa viwanja kulingana na Mpango ulioidhinishwa na Mamlaka husika (Cadastral Survey). Pia usanifu (*Engineering design*) wa matangi ya maji safi, mabwawa ya maji taka na mfumo (network) wa kusambaza maji safi na kukusanya taka umekamilika. Kwa upande wa barabara, usanifu umefanyika kwa kipande cha urefu wa Km 1 ambapo sehemu yanye urefu wa meta 400 tayari imejengwa kwa kiwango cha lami mpaka kilipo kiwanda cha Viuadudu (Biolarvicides).

**Mheshimiwa Spika**, miundombinu inayohitajika katika Eneo la mradi ni barabara, kituo cha kupoozea umeme, mtandao wa nyaya za kusambaza umeme, matanki ya kuhifadhi maji safi, mabwawa ya kutibu maji yaliyotumika na mitandao ya mabomba kwa ajili ya kusambaza maji safi na kukusanya maji taka. Makadirio ya gharama za kujenga miundobinu hiyo ni Shilingi **Bilioni 16.4.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa faida zitakazopatikana iwapo mradi huu utatekelezwa kuwa, ni kivutio kwa wawekezaji wengi. Mradi huu ukikamilika unatarajiwa kuwa na miundombinu yote wezeshi kwa ajili ya uwekezaji. Aidha, eneo hili la Viwanda lipo katika barabara kuu ya Dar es salaam Morogoro hivyo kurahisisha usafirishaji wa malighafi na bidhaa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea maelezo kuhusu Changamoto za utekelezaji wa mradi huu kuwa ni ukosefu wa fedha jambo linalokwamisha utekelezaji wake. Mahali eneo la TAMCO lilipo tayari ni kivutio muhimu kwa wawekezaji wetu. Hili linajidhihirisha kwasababu ya kuwa na wawekezaji walionyesha nia ya kuwekeza pamoja na kuwa bado miundombinu yake haijakamilika. Kamati inaishauri Serikali ipeleke fedha zilizosalia kwa ajili utekelezaji wa mradi huu ili uweze kukamilika kwa wakati kama ilivyopangwa. Pia miradi ya aina hii itekelezwe katika maeneo mengine ya uwekezaji yaliyotengwa katika sehemu mbalimbali nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia ilitembelea katika kiwanda cha Saruji Tanga (Tanga Cement PLC) na kuelezwa baadhi ya changamoto zinazowakabili kama ifuatavyo:-

i) **Kutokuwepo kwa nishati ya Umeme ya uhakika.**

**Meshimiwa Spika,** kukatika mara kwa mara kwa nishati hii muhimu kunawapunguzia uwezo wa kuzalisha lakini pia kunasababisha uharibifu wa malighafi na mitambo;

ii) **Serikali kutoa motisha kwa baadhi ya wazalishaji wa Saruji**

**Meshimiwa Spika,** Uamuzi wa Serikali kutoa motisha kwa baadhi ya wazalishaji wa Saruji huku wengine wakiachwa unalalamikiwa na wadau wa sekta hiyo. Hatua hii itasababisha baadhi ya wazalishaji wa Saruji kuzalisha

kwa gharama kubwa hivyo kuwapunguzia ushindani katika Soko;

iii) **Kuzuia uingizaji wa Makaa ya Mawe kutoka nje ya nchi**

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imezuia kuagiza makaa ya mawe kutoka nje ya nchi wakati yaliyopo hayatoshelezi mahitaji. Hatua hii imeongeza bei ya Makaa ya mawe ya yanayozalishwa hapa nchini. Pamoja na ukweli kuwa makaa ya mawe yanayoyazalishwa hayatoshelezi mahitaji lakini pia usafirishaji wake kutoka Mkoani Ruvuma unakabiliwa na changamoto ya ubovu wa miundombinu. Miundombinu ya Reli iliyopo haina uwezo wa kuhimili mizigo mizito. Barabara inayokwenda mahali machimbo yalipo hupitika kwa shida sana wakati wa masika. Makaa ya mawe yanachangia asilimia **70** ya gharama zote za kuzalishaji wa Saruji hivyo kuongeza sana gharama za uzalishaji; na

iv) **Serikali iliingia Mkataba na Kampuni ya Tanga Cement kwa kupitia TIC**

**Meshimiwa Spika,** katika Mkataba huo Serikali iliahidi kutoa msamaha wa Kodi ya Zuio baada ya kampuni kukidhi vigezo vilivyowekwa kisheria na *Tanzania Investment Centre* (TIC). Hadi kufikia Machi, 2017 hakuna Tangazo lililotolewa kwenye Gazeti la Serikali, ili

kutoa msamaha uliokuwa ulioahidiwa pamoja na ukweli kwamba Mkataba huo ulisainiwa mwaka 2009.

## 3.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MAAGIZO YA KAMATI KUHUSU BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa kupitia na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Kamati ilitoa ushauri kwenye maeneo mbalimbali. Naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imejitahidi kuzingatia ushauri wa Kamati, hata hivyo kuna maeneo ambayo serikali haikuyatekeleza ipasavyo kama inavyoainishwa kwenye taarifa hii.

i) ***Serikali iweke kipaumbele katika kuweka mazingira wezeshi kwa viwanda vinavyoajiri watu wengi, mfano viwanda vya nguo vinavyotumia pamba, viwanda vya korosho, kahawa na mbegu za mafuta.*** Maelezo yaliyotolewa na Wizara ni kuwa imetekeleza agizo hili kwa kuwahimiza Tawala za Mikoa kutenga maeneo kwa ajili ya ujenzi wa viwanda. Kamati haijaridhishwa na utekelezaji huu kwani utengaji wa maeneo tu hatuoshi. Hivyo basi Kamati inashauri kuwa maeneo yanayotengwa yapimwe na kuwekewa miundombinu ili kuyafanya kuwa tayari ili muwekezaji akija akute eneo lipo tayari kwa yeye kuanza uwekezaji wake.

ii) ***Serikali ihakikishe viwanda vya ndani vinapatiwa mazingira safi ya ushindani*** Maelezo ya Serikali ni kuwa wameandaa waraka maalumu na kuwakilisha kwenye Baraza la Mawaziri ikipendekeza mbinu na mikakati ya kupambana na matatizo ya ushinda katika sekta ya ushindani. Kamati hairidhishwi na kasi ya utekelezaji wa agizo hili, na inashauri Serikali ichukue hatua za makusudi tena za haraka katika kuhakikisha mazingira ya ushindani yanakuwa safi kwa manufaa ya mlaji, kwani pia yatavutia wawekezaji kuja kuwekeza au kupanua uwekezaji wao kwa wale waliopo sokoni.

iii) ***Serikali iongeze hisa kwa viwanda ambavyo ina hisa chache. Hatua hii itasaid-ia kulinda maslahi ya Serikali na wafanyakazi kama ilivyofanyika kwa kiwanda cha General tyre. Viwanda hivyo ni TANELEC na URAFIKI na vinginevyo.*** Maelezo ya serikali kuhusu kiwanda cha TANELEC, ni kwamba Wizara inajadiliana na Msajili wa Hazina juu ya njia bora ya kuongeza hisa za Serikali. Kuhusu Kiwanda cha URAFIKI Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) alipewa jukumu la kukagua Hesabu za Kiwanda hicho na Taarifa siyo nzuri. Kamati inaendelea kusisitiza utekelezaji wa agizo hili, kwani hatua zilizochukuliwa mpaka sasa si za kuridhisha.

iv) ***Serikali itekeleze miradi ya Liganga na Mchuchuma ambayo ni miradi ya kipaumbele kwenye Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano 2020/2021 ili kuchochea kukua kwa viwanda hivi.*** Maelezo ya Serikali ni kuwa yalitolewa maelekezo na Baraza la Mawaziri kuwa mkataba wa Miradi hii upitiwe upya. Kamati ya Makatibu Wakuu iliundwa nakupitia mkataba huo na kutoa mapendekezo ya vivutio kwa kuzingatia maslahi ya Taifa. Mapendekezo hayo yanasubiri kujadiliwa na Kamati ya Taifa ya Uwekezaji kabla ya kujadiliwa na muwekezaji. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi hii kwani utekelezaji wake utachochea sekta ya Viwanda nchini.

## 4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

### 4.1 Uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2017/2018

**Makisio ya Maduhuli**

**Mheshimiwa Spika,** kamati ilijulishwa kuwa katika mwaka wa fedha 2017/2018 Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji imepanga kukusanya shilingi bilioni **20** kutokana na ada za

leseni, nyaraka za zabuni na faini kwa kukiuka Sheria ya Leseni. Uchambuzi wa Kamati uulibainisha mambo yafuatayo:-

i) Lengo lililowekwa ni kukusanya asilimia **16** ya fedha zinazoombwa katika mwaka wa fedha 2017/2018, kiasi hiki ni pungufu kwa asilimia **8** ya lengo la makusanyo ya asilimia **24** mwaka wa fedha 2016/2017.

ii) Makadirio ya makusanyo ya mwaka wa fedha **2017/2018** ni sawa na makadirio ya mwaka wa fedha unaoishia ambayo hayakufikiwa aidha kwa sababu hayakuwa halisi au juhudi za ukusanyaji hazikuwa nzuri.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaona ni vyema Wizara ikajiwekea lengo la makusanyo kwa kuzingatia uwezo wao wa kukusanya. Aidha, Serikali iangalia upya changamoto zilizopelekea kutofikia malengo hayo na ifanye jitihada za kukabiliana na changamoto hizo ili kuhakikisha wanafikia malengo wanayojiwekea hususani katika kipengele cha uuzaji wa nyaraka za zabuni.

**Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2017/2018**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara imetengewa jumla ya Shilingi **122,215,109,201** kwa ajili ya matumizi ya Kawaida na miradi ya Maendeleo kwa mafungu **44** na **60.** Kati ya fedha hizo Shilingi

**80,190,377,451** sawa na asilimia **65.6** ni kwa ajili ya matumizi ya Maendeleo na Shilingi **42,024,731,750** sawa na asilimia **34.4** ya fedha zote zinazoombwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Mchanganuo huu ni kwa mafungu yote mawili (2) Fungu **44-**Viwanda na Fungu **60-**Biashara na Uwekezaji. Bajeti inayopendekezwa ya Shilingi **122,215,109,201** ni zaidi kwa asilimia **49.2** ikilinganishwa na Shilingi **81,871,992,000** zilizoidhinishwa katika mwaka wa fedha **2016/2017**.

## i) FUNGU 44 -VIWANDA

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji Fungu **44-Viwanda** imetengewa jumla ya shilingi **98,012,869,451** kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Wizara. Kiasi hiki ni sawa na asilimia **80** ya shilingi **122,215,109,201** ya bajeti yote ya Wizara. Kati ya fedha hizo shilingi **24,172,492,000** sawa na asilimia **24.7** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shillingi **73,840,377,451** sawa na asilimia **75.3** ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo. Kati ya shilingi **24,172,492,000** fedha zilizoombwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, Shilingi **19,603,120,000** ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi na Shilingi **4,569,372,000** ni Bajeti ya Matumizi Mengineyo(OC).

## ii) FUNGU 60- BIASHARA NA UWEKEZAJI

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha **2017/2018,** Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Fungu **60**-**Biashara na Uwekezaji**, imetengewa jumla ya Shilingi **24,202,239,750** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kiasi hiki ni sawa na asilimia **20** ya bajeti yote ya Wizara, shilingi **122,215,109,201.** Kati ya fedha hizo shilingi **17,852,239,750** sawa na asilimia **73.8** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shillingi **6,350,000,000** sawa na asilimia **26** ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo. Kati ya shilingi **17,852,239,750** fedha zilizoombwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida Shilingi **15,964,331,000** sawa na asilimia **66** ni kwa ajili ya Mishahara ya watumishi. Kiasi kinachosalia Shilingi **1,887,908,750** sawa na asilimia **8** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC).

## 5.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imekuwa na mwenendo usioridhisha katika kutoa fedha hasa zile za miradi ya mendeleo hivyo kuchelewesha utekelezaji wake. Aidha kiasi kinachopelekwa ni kidogo hivyo kushindwa kuanza mchakato wa utekelezaji. Kwa mara nyingine tena, Kamati inaishauri Serikali itoe fedha za maendeleo kwa wakati ili kurahisisha utekelezaji wa miradi iliyokusudiwa.

### 5.1 Sekta ya Viwanda

**Mheshiwa Spika,** nishati ya Umeme ni muhimu sana kwa Uchumi unaotegemea viwanda kama ambavyo Serkali yetu inakusudia. Kamati ilipata fursa ya kuvitembelea baadhi ya viwanda, miongoni mwa changamoto kubwa zilizotajwa ni pamoja na kukosekana mara kwa mara kwa nishati hii muhimu. Wakati mwingine hata pale inapopatikana kuwa katika kiwango kidogo hivyo kushindwa kuendesha Mitambo. Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya usambazaji wa nishati ya umeme wa kutosha na wa uhakika.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua uwepo wa mipango mizuri ya Serikali katika kukabiliana upungufu wa Nishati ya Umeme nchini lakini utekelezaji wake umekuwa wa kusuasua. Kamati inaishauri Serikali ikamilishe mapema mipango yake ya

kuongeza nishati hii kwa ajili ya ujenzi wa Uchumi wa viwanda nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imesitisha uagizaji wa makaa ya mawe kutoka nje ya nchi lakini makaa yanayozalishwa hayatoshelezi mahitaji ya sasa ya soko. Kamati inaishauri Serikali kwamba wakati inahamasisha uwekezaji katika uchimbaji wa makaa ya mawe yaliyopo hapa nchini, iruhusu uagizaji wa makaa ya mawe kutoka nje ya nchi ili uzalishaji katika viwanda vinavyotumia nishati hii usikwame katika kipindi hiki cha mpito.

**Mheshimiwa Spika,** kamati inaishauri serikali iangalie namna bora ya kuiwezesha Benki ya Rasilimali Tanzania (Tanzania Investment Bank) ili ifungue matawi Mikoani lakini pia kuiongezea Mtaji, hatua ambayo itasaidia Mikopo kuwafikia watanzania walio wengi. Pia Kamati inaishauri Serikali iitumie Benki hii katika kutafuta fedha za miradi mikubwa ya maendeleo kutoka nje ya nchi ili kujenga miradi muhimu ya miundombinu ya barabara, reli, bandari na Viwanja vya ndenge.

## 5.2 Sekta ya Biashara

**Mheshimiwa Spika,** kumekuwa na ushindani usio wa haki kati ya bidhaa zinazozalishwa hapa nchini na zile zinazoagizwa kutoka nje ya nchi. Sababu kubwa inayotajwa ni baadhi ya

wafanyabiashara wasiowaaminifu kuingiza bidhaa hizo kwa njia za panya na kukwepa kulipa Kodi. Malalamiko pia yapo kuhusu Viwango vidogo vya kodi vinavyotozwa kwa baadhi ya bidhaa zinazoingia kutoka nje ya nchi. Hali hii inapelekea bidhaa hizo kuuzwa kwa bei rahisi kuliko zile zinazozalishwa hapa nchini. Kamati inaishauri Serikali kuimarisha udhibiti katika mipaka yake ili bidhaa zote zinazoingizwa kutoka nje ya nchi zilipiwe Kodi stahiki.

**Mheshimiwa Spika,** kumekuwa na changamoto ya kukosekana kwa Soko kwa baadhi ya bidhaa zinazotengenezwa hapa nchini, kwa sababu ya kukosa ubora au gharama za uzalishaji kuwa juu. Mfano ni Kiwanda cha Viadudu Kibaha ambacho kinakabiliwa na ukosefu wa Soko kwa bidhaa zake na hivyo kusitisha uzalishaji. Kamati inaishauri Serikali kwamba ilikuepuka kuwa na viwanda vingi ambavyo havizalishi kila anayekusudia kuanzisha Kiwanda kipya kufanya utafiti wa kutosha kuhusu soko la bidhaa husika.

**Mheshimiwa Spika**, wafanyabishara wamelalamikia wingi wa mamlaka za udhibiti ambazo zinafanya kazi zinazofanana na hivyo kuonekana kama kero kwa wafanyabiashara. Mfano TBS, TFDA, OSHA, FIRE, n.k. Kamati inaendelea kusisitiza Serikali izipitie upya sheria za uanzishaji wa mamlaka hizi na kuona uwezekano wa kaguzi hizo kufanywa na mamlaka moja ila kuwe na uwezekano wa kushea majibu kwa mamlaka nyingine.

Aidha, gharama za kaguzi zipitiwe upya na kupunguzwa kwa kuwa zimelalamikiwa na wafanyabiashara wengi kuwa ni kikwazo.

## 5.3 Sekta ya Uwekezaji

**Mheshimiwa Spika,** kukinzana kwa sheria za uwekezaji na sheria ya Ongezeko la Thamani (VAT) hususani kwa uwekezaji wa kimkakati kama wawekezaji wa viwanda vya madawa ya kilimo, mifugo, na vyandarua vya kupambana na ugonjwa wa Malaria. Kutozwa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) katika uwekezaji wa namna hii kunapunguza ushindani na bidhaa shindani zinazoingia kutoka nje ya nchi. Kamati inaishauri Serikali, kwamba uwekezaji wa kimkakati upate fursa ya kuwa *zero rated,* hatua hii itaongeza ushindani na bidhaa zinazoingia kutoka nje lakini pia kulinda viwanda vya ndani.

**Mheshimiwa Spika,** Bado kuna malalamiko mengi kutoka kwa wawekezaji kuhusu urasimu usio na tija wakati wa kupata taarifa na vibali mbalimbali kwa ajili ya uwekezaji. Kamati inaishauri Serikali iangalie upya mazingira ya kufanya biashara hapa nchini ili kuwavutiwa wawekezaji wengi.

**Mheshimiwa Spika**, kwa uwekezaji wa kimkakati kama Miradi ya Liganga na Mchuchuma; Mradi wa Magadi Soda wa Ziwa Natron na Magadi Soda wa Engaruka Serikali iharakishe

kutangaza katika Gazeti la Serikali ili misamaha ya kodi iliyoombwa ipatikane kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** mradi wa General Tyre kamati inapongeza hatua ya Serikali ya kuamua kuutekeleza kwa kutafuta mwekezaji. Kamati inaishauri Serikali iongeze kasi ya utekelezaji, kwa vile kukamilika kwake kutaongeza mchango katika pato la Taifa lakini pia kuongeza ajira.

**Mheshimiwa Spika,** wawekezaji wamelalamikia suala la utoaji wa vivutio vya uwekezaji kuwa hauko sawa miongoni mwa wawekezaji. Wawekezaji kutoka nje ya nchi wamekuwa wakipatiwa vivutio vingi zaidi hivyo kuwakatisha tamaa wawekezaji wa ndani wanapotaka kuwekeza. Mfano muwekezaji Dangote amepewa gesi na makaa yamawe kwa bei nafuu zaidi wakati wawekezaji wa aina yake hawajapata. Kamati inaishauri Serikali kuwa motisha ambazo zinaweza kutolewa kwa wawekezaji wote wa ndani na nje ni vizuri wote wakapatiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kuongeze kasi ya uwekaji wa miundombinu wezeshi katika Mradi wa NDC-*Industrial Park (TAMCO-Kibaha)*, Kamati inaamini kwamba mradi huu ukikamilika utakuwa kivutio kwa wawekezaji wengi lakini pia iangaliwe namna ya kuanzisha miradi mingine ya aina hii katika maeneo mengine nchini.

**Mheshimiwa Spika,** wadau wengi wa uwekezaji wakiwemo wafanyabiashara na wenyeviwanda wameendelea kulalamikia uwepo wa utitiri wa kodi na kuongezeka kiholela kwa kodi mbalimbali katika viwanda na biashara mbalimbali. Kwa mfano kuwekwa kwa VAT kwenye huduma ya mizigo inayopita bandarini (*VAT on auxiliary service on transit goods*) imepunguza sana biashara katika Bandari ya Dar es Salaam. Kamati inaendelea kuishauri Serikali izipitie upya kodi na tozo hizi kwa lengo la kuzipunguza ili kuhamasisha uwekezaji nchini na kuharakisha ujenzi wa Viwanda katika nchi yetu.

## 6.0 HITIMISHO:

**Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Awamu ya Tano imejielekeza katika kujenga mazingira bora ya uwekezaji nchini ili kujenga nchi ya Viwanda. Kamati inaunga mkono na kupongeza hatua zote zinazochukuliwa na Serikali katika kuboresha mazingira ya uwekezaji. Kamati inaiomba Serikali iongeze juhudi za kuweka mazingira ya uwekezaji nchini kuwa ya kuvutia. Kufanya hivyo kutaharakisha kuifanya Tanzania kuwa nchi ya Viwanda nay a kipato cha kati ifikapo mwaka 2025.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapenda kumshukuru Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji Mhe. Charles Mwijage (Mb), Makatibu Wakuu, Dr. Adelhelm Meru na Prof. Adolph Mkenda, pamoja na wataalamu wote wa Wizara ya Viwanda, Biashara na

Uwekezaji kwa kuwa tayari kutoa ufafanuzi na kupokea maoni na ushauri wa Wajumbe wa Kamati yangu wakati wote wa mjadala wa makadirio haya. Ni matarajio ya Kamati kuwa ushirikiano huu utaendelea katika kipindi cha mwaka ujao wa Fedha.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee kabisa, napenda kuwashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira ambao wameweza kutoa maoni na michango mbalimbali katika kuboresha makadirio haya ili hatimaye yaletwe mbele ya Bunge hili tukufu. Orodha yao ni kama inavyosomeka hapa chini.

| | | |
|---|---|---|
| (i) | Mhe. Stanslaus Haroon Nyongo Mb | Mwenyekiti |
| (ii) | Mhe. Vicky Passcal Kamata, Mb | Mjumbe |
| (iii) | Mhe. Salim Hassan Turky, Mb | Mjumbe |
| (iv) | Mhe. Kalanga Julius Laizer, Mb | Mjumbe |
| (v) | Mhe Dkt. Dalaly Peter Kafumu | Mjumbe |
| (vi) | Mhe. Khatib Said Haji, Mb | Mjumbe |
| (vii) | Mhe. Tauhida Cassian Gallos, Mb | Mjumbe |
| (viii) | Mhe. Munira Mustafa Khaibu, Mb | Mjumbe |
| (ix) | Mhe. Anthony Calist Komu, Mb | Mjumbe |
| (x) | Mhe. Godbless Jonathan Lema, Mb | Mjumbe |
| (xi) | Mhe. Dkt. Mary Machuche Mwanjelwa,Mb | Mjumbe |
| (xii) | Mhe. Lameck Okambo Airo, Mb | Mjumbe |
| (xiii) | Mhe. Hawa Subira Mwaifunga, Mb | Mjumbe |

(xiv) Mhe. Balozi Dkt Diodorus Kamala, Mb — Mjumbe

(xv) Mhe. Jesca David Kishoa, Mb — Mjumbe

(xvi) Mhe. Mbarouk Salim Ali, Mb — Mjumbe

(xvii) Mhe. Mussa Ramadhani Sima, Mb — Mjumbe

(xviii) Mhe. Anatropia Lwehikila Theonest, Mb — Mjumbe

(xix) Mhe. Faida Mohammed Bakar, Mb — Mjumbe

(xx) Mhe. Suleiman Ahmed Sadick, Mb — Mjumbe

(xxi) Mhe Ibrahim Hassanali Raza, Mb — Mjumbe

(xxii) Mhe. Abdulaziz Mohamed Abood, Mb — Mjumbe

(xxiii) Mhe. Dkt. Raphael MMasunga Chegeni, Mb — Mjumbe

(xxiv) Mhe. Sylvestry Francis koka, Mb — Mjumbe

(xxv) Mhe. Gimbi Dotto Massaba, Mb — Mjumbe

(xxvi) Mhe. Martha Mosses Mlata, Mb — Mjumbe

(xxvii) Mhe. Joyce John Mukya, Mb — Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, naomba nikushukuru sana wewe kwa uongozi wako thabit kwa Bunge la 11; niwashukuru pia Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuratibu na kusimamia vema shughuli za Bunge. Aidha, napenda pia kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas D. Kashililah; Mkurugenzi wa Idara ya Kamati Bw. Athumani Hussein; Mkurugenzi msaidizi Sehemu ya Fedha na Uchumi Bw. Michael Chikokoto; Makatibu wa Kamati Bw. Wilfred Magova na Bi. Zainab Mkamba na Msaidizi wa Kamati Bi Paulina Mavunde kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi taarifa hii kukamilika.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kusema haya, sasa naliomba Bunge lako tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fungu **44** na **60**, kwa mwaka wa fedha **2017/2018** kiasi cha shilingi ***122,215,109,201*** ambapo shilingi ***42,024,731,750*** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi ***80,190,377,451*** ni kwa ajili matumizi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Stanslaus Haroon Nyongo, (Mb)

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA**

17 Mei, 2017